
# Mtazamo wa Viongozi wa Biashara kuhusu Mazingira ya uwekezaji Tanzania




BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy

**BLP-2013**

**DAR ES SALAAM**

**IRWIN GRAYSON ASSOCIATES**

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ufupisho | 4 |
| 2. | Utangulizi | 6 |
| 3. | Tathmini ya mazingira wezeshi | 6 |
| 4. | Mantiki ya utafiti | 11 |
| 5. | Mbinu ya utafiti | 11 |
| 6. | Mapitio | 12 |
| 7. | Tathmini mahali ilipo biashara | 19 |
| 8. | Gharama za urasimu | 20 |
| 9. | Kodi | 21 |
| Rejea | | 22 |

## 1. Ufupisho

Huu ni utafiti wa tano kuhusu maoni/mtazamo wa wafanyabiashara Tanzania. Wafanyabiashara hao waliulizwa kuhusu:


- Mambo mbalimbali yanayosaidia mazingira wezeshi katika kufanya biashara;
- Mambo yanayosababisha ugumu wa kufanya biashara;
- Vizingiti vinavyosaidia kufanyika kwa biashara;
- Vizingiti vinavyokwamisha kufanyika kwa biashara;
- Maoni kuhusu jinsi serikali inavyosaidia kuondoa kila aina ya kikwazo;
- Maoni iwapo kila kizingiti kitakwamisha jitihada za uwekezaji kwa siku za usoni; na
- Tathmini ya gharama zinazohusika katika kutimiza matakwa ya sheria na urasimu.

  Utafiti unaonesha kwamba mambo yanayokwamisha uendeshaji na ukuaji wa biashara ni:

- Umeme
- Kiwango cha kodi
- Rushwa
- Ulipaji wa kodi

  Ukosefu wa umeme ni tatizo kubwa likifuatiwa na barabara mbovu ingawa kwa mwaka 2012 barabara lilikuwa ni tatizo la sita. Kwa mwaka 2010, suala la upatikanaji wa maji halikuwa tatizo kubwa ingawa bado linaendelea kuonekana ni kikwazo kwa wafanyabiashara. Upatikanaji wa fedha, ambalo lilionekana ni tatizo mwaka 2009 na 2010, kwa mwaka 2011 kulikuwa na maendeleo mazuri ingawa mwaka 2012 hali ilikuwa mbaya.


**Kielelezo 1: Mambo yanayochangia ugumu wa kufanya biashara kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo**




Utafiti huu unataka kuonesha iwapo serikali inafanya jitihada za kuyatafutia ufumbuzi matatizo haya. Ugumu wa kufanya biashara unaosababishwa na


kila tatizo na jinsi serikali inavyofanya jitihada za makusudi kuyatafutia ufumbuzi matatizo hayo huunganishwa pamoja na kuwa kigezo kimoja cha 'mazingira wezeshi.'

Angalia katika kielelezo kifuatacho kwamba namba ikiwa ndogo, ndivyo ukubwa wa kipaumbele ulivyo.




Mambo ambayo serikali inapaswa kuyapa kipaumbele yanaonyeshwa upande wa kulia wa kielelezo namba 3, ambacho pia kinaonyesha jinsi vipaumbele vilivyobadilika tangu 2008. Umeme na rushwa vinaendelea kuongoza katika orodha hiyo. Suala la kodi limejitokeza zaidi -- hasa jinsi linavyotekelezwa – pia limejitokeza katika orodha hiyo.

**Kielelezo 3 : Mabadiliko ya vipaumbele**




Kutokuwepo kwa kikwazo chochote katika orodha hii hakuna maana kwamba serikali inaweza kupuuza, bali inatakiwa kufanya kila jitihada kupunguza vikwazo vinavyoathiri ukuaji wa biashara. Jitihada hizo ni lazima ziendelee ama sivyo hali hiyo itabidi iwe ni kipaumbele kwa siku zijazo. Lazima ieleweke wazi kwamba vigezo hivi ni vipimo linganishi tu na siyo vipimo mahsusi. Kwa hiyo tofauti kati ya kipimo linganishi kimoja na kingine ni ndogo mno.

## 1. Utangulizi

Hii ni ripoti ya tano ya maoni/mtazamo wa wafanyabiashara nchini. Inaelezea kwa ufupi maoni/mtazamo wao kuhusu mazingira wezeshi na wajibu wa serikali wa kurahisisha uendeshaji wa biashara. Lengo la ripoti hii ni kuibua mjadala kati ya sekta binafsi na serikali na kuweka wazi baadhi ya mambo yanayopaswa kupewa kipaumble ili kuimarisha na kuboresha mazingira wezeshi ya uendeshaji wa biashara.

Ripoti hii iliandaliwa na Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (BEST-AC) ambao jukumu lake ni kusaidia mashirika mbalimbali yaliyo chini ya sekta binafsi(PSOs) kuwa na mjadala kati ya sekta hiyo na serikali ili kuleta mabadiliko ya kisera kwa lengo la kuimairisha mazingira ya biashara nchini.

Tangu mwaka 2003 Benki ya Dunia ilipochapisha kwa mara ya kwanza ripoti yake ya "Uendeshaji Biashara", taasisi hiyo ya *Bretton Woods* imekuwa ikisisitiza kwamba kuimairishwa kwa mazingira wezeshi kutainua kiwango cha uwekezaji kwa upande wa sekta binafsi, kujenga uchumi, kukuza ajira, na hatimaye kupunguza umaskini.

Benki ya Dunia pamoja na nchi nyingine wahisani zinaamini kwamba njia pekee kwa serikali kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara ni kuihusisha sekta binafsi kupitia ushauri na mijadala mbalimbali, lengo kuu likiwa ni kuelewa na kutafakari mahitaji na vipaumbele vya sekta hiyo. Hicho ndicho kiini cha benki hiyo kuisaidia BEST-AC, ambayo nayo inayasaidia mashirika yaliyo chini ya sekta binafsi.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwa uwazi kwamba maoni ya wafanyabishara hayajabadilika kwa kiasi kikubwa tangu mwaka 2009 hadi 2012, hali ambayo inashabihiana na tathmini ya ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu "Uendeshaji Biashara" pamoja na tafiti nyingine za taasisi kama vile *Global Competitiveness Index*. Taswira inayojengwa na hali halisi ya mazingira ya uendeshaji biashara nchini ni kwamba mambo bado hayajabalika. Hii si taswira nzuri kwa sababu serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa kuimarisha mazingira wezeshi ya uendeshaji biashara kwa kuunda Sera mahsusi na vikosi kazi mbalimbali katika wizara nyeti ambavyo vimetengewa majukumu maalum.

## 2. Tathmini ya mazingira wezeshi

Benki ya Dunia hufanya tafiti za viashiria mbalimbali na kuzichapisha katika ripoti zake za "Uendeshaji Biashara" za kila mwaka.

Ripoti hizo huelezea idadi ndogo ya viashiria hivyo. Nchi nyingi huzingatia maoni yanayotolewa na ripoti hizo na kuzifanyia kazi kwa kupunguza urasimu

ili kuleta mabadiliko. Kwa hakika, nchi nyingi hujiwekea malengo ya kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara. Inawezekana kutilia mkazo viashiria viwili au vitatu ili kuleta mabadiliko katika kurahisisha uendeshaji wa biashara (hasa, ulinganisho). Hata hivyo, mtazamo wa sekta binafsi huenda ukawa kwamba hakuna mabadiliko yaliyokwishafanyika.

Katika ripoti ya "Uendeshaji Biashara" ya 2013, Tanzania inachukua nafasi ya 134, hali inayoonesha imeshuka ikilinganishwa na mwaka jana. Kwa kuzingatia kwamba mwaka 2011 Tanzania ilijiwekea lengo la kushika nafasi ya 99, hali hiyo ya kuwa nafasi ya 134 inakatisha tamaa. Kielelezo kifuatacho, kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia ya "Uendeshaji Biashara" 2013, kinaonesha Tanzania ilifanya jitihada kubwa za kupunguza masharti ya kuanzisha biashara. Ingawa Benki ya Dunia haisemi chochote, inaelekea Tanzania imefanya vizuri zaidi katika suala la usajili wa mali.

**Jedwali 1. Ulinganisho wa Uendeshaji Biashara Tanzania**

| | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 |
|---|---|---|---|---|---|
| | (DB 2009) | (DB 2010) | (DB 2011) | (DB 2012) | (DB2013) |
| Urahisi wa kufanya biashara | 126 | 131 | 128 | 127 | 134 |
| Kuanzisha biashara | 109 | 120 | 122 | 123 | √113 |
| Suala la leseni | 172 | 178 | 179 | 176 | *174 |
| Usajili wa mali | 142 | 145 | 151 | 158 | 137 |
| Ulipaji kodi | 109 | 119 | 120 | 129 | 133 |
| Kutimiza mikataba | 33 | 31 | 32 | 36 | 36 |
| Biashara na nchi jirani | 103 | 108 | 109 | 92 | *122 |


**Vyanzo: Ripoti za Uendeshaji Biashara za Benki ya Dunia 2008-2012**

Pengine ni vizuri kulinganisha jitihada za Tanzania na nchi jirani. Kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia ya `Uendeshaji Biashara' ya mwaka 2010, Rwanda ndiyo iliyochukua nafasi ya kwanza duniani mwaka 2009 kwa kufanya mageuzi makubwa katika kuimarisha mazingira ya uendeshaji biashara. Nchi hiyo ilipanda nafasi 76 na kuwa ya pili kwa kufanya mageuzi mwaka 2010 baada ya kupanda nafasi 9. Hata hivyo, nchi hiyo imeshindwa kushikilia nafasi hiyo baada ya kushuka nafasi yake mwaka 2012. Pengine imekuwa ni kichocheo kwa nchi nyingine kufanya vizuri. Mtu anapoangalia kielelezo kifuatacho itaonekana kana kwamba nafasi ya Tanzania imekuwa haibadiliki.



Katuni imechorwa na Samuel Mwamkinga

**Jedwali 4: Ulinganisho wa "Uendeshaji Biashara'**




**Vyanzo: Ripoti za 'Uendeshaji Biashara' za Benki 2006-2013**

Ingawa juhudi za Benki ya Dunia zinathaminiwa na watunga sera kwa kuonesha maeneo yanayohitaji maboresho na pia kukuza mjadala, benki hiyo haitoi suluhisho la mambo yote. Hali kadhalika, kuwahamasisha watu wengi kuanzisha biashara au kuwahamasisha watu wengi kujiunga na uchumi rasmi au kuanzishwa kwa vitega uchumi kutategemea zaidi mtazamo wa kufanya biashara kwa urahisi na wala siyo kwa kuzingatia kama ilivyoelezwa kwenye ripoti ya Benki ya Dunia ya `Uendeshaji Biashara'.

Jukwaa la Uchumi Duniani pia hufanya tafiti na kuchapisha hali ya mwenendo wa kibiashara, hasa kwa kuangalia kigezo cha ushindani. Ripoti hiyo iitwayo `Global Competitiveness Index' huchapishwa kila mwaka.

**Kielezo 5: Ushindani wa kibiashara duniani**





***Vyanzo: Schwab,K, (2011, 2012)***

Kiwango cha Tanzania kimekuwa kikishuka polepole. Mwaka 2009/10 ilishika nafasi ya 100. Ilipofikia mwaka 2010/11 ikashuka hadi nafasi ya 113. Mwaka 2011/12 ilishuka tena na kushika nafasi ya 120 ambayo bado inaishikilia hadi mwaka 2012/13. Pamoja na kulinganisha nchi, Jukwaa la Uchumi Duniani pia hutoa ulinganisho kwa kila aina ya kigezo inachotumia. Vigezo hivyo vimeoneshwa kwenye kielelezo cha 5. Inaoneshwa kwamba Tanzania imeshikilia nafasi ya 120 kwa miaka miwili mfululizo. Kiwango cha juu kwa kila kigezo ni 7. Kwa hiyo, haishangazi kwamba kigezo kibaya kwa Tanzania kiko kwenye eneo la miundombinu ambalo ni 2.3.

Tanzania sasa hivi ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ingawa itabidi ifanye jitihada kubwa kuifikia Uganda.

Ripoti ya ***`Global Competitivenes'*** pia inawauliza wafanyabiashara, hasa kuhusu matatizo wanayokumbana nayo katika uendeshaji biashara. Kwa kuuliza swali hilo, watu wanaohojiwa wanapewa orodha ya mambo mbalimbali (kama ilivyooneshwa kwenye kielelezo) na kutakiwa kuchagua na kulinganisha mambo matano yanayosababisha ugumu wa kufanya biashara. Kielelezo cha 6 kinaonesha wazi matatizo makubwa katika uendeshaji wa biashara kuwa ni rushwa, upatikanaji wa fedha na ubovu wa miundombinu. Matatizo hayo yameoneshwa kwa uwazi zaidi katika utafiti uliofanyika.

**Kielelezo 6: Matatizo ya uendeshaji biashara**




**Chanzo: Schwab,K, (2012)**

Kila mwaka shirika la Transparency International huchapisha ripoti yake kuhusu suala la rushwa. Ingawa Tanzania haifanyi vizuri katika mapambano dhidi ya tatizo hilo, hata hivyo inashika nafasi ya pili kutoka nchi jirani ya Rwanda ambazo zote ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Zipo nchi 174 zilizomo katika tathmini hiyo ambazo kipimo chake ni 100.




*Katuni imechorwa na Idd Marumba*

**Jedwali 2. Kiwango cha rushwa kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**

| | Rwanda | Tanzania | Uganda | Kenya | Burundi |
|---|---|---|---|---|---|
| | Rank | Score | | | |
| Ulinganisho | 50 | 102 | 130 | 139 | 165 |
| Tathmini | 53 | 35 | 29 | 27 | 19 |

**Chanzo: Transparency International**

## 4. Matinki ya utafiti

Kuwepo kwa mashirika kama vile Benki ya Dunia na Jukwaa la Uchumi Duniani yanayofanya utafiti kutathmini matatizo yanayoikabili sekta ya biashara, inaweza kuonekana kwamba hakuna haja tena ya kufanya utafiti au uchambuzi. Utafiti huu ni tofauti:

- Mtazamo na uhalisia kwa kawaida ni vitu viwili tofauti – na watu hutenda kutokana na mitazamo yao, ingawa mitazamo hiyo si sahihi. Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kwa taasisi na serikali kuelewa mitazamo ya wafanyabiashara. Hii, kwa maana pana zaidi, itasaidia kuelewa maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji hatua zichukuliwe. Katika maeneo ambako tayari hatua zimeshachukuliwa serikali inaweza kuimarisha mawasiliano yake na sekta binafsi.

- Utafiti huu unatenganisha mambo muhimu kwa sekta maalum. Yapo mambo kadhaa ambayo kwa pamoja yanaleta mazingira wezeshi, ingawa si yote ni muhimu kwa kila biashara au yanasababisha uendeshaji wa biashara kuwa mgumu. Jambo ambalo ni muhimu kwa uendeshaji wa biashara siyo lazima liwe ni jambo linalosababisha ugumu wa biashara ingawa upo uhusiano wa karibu.

- Utafiti huu siyo tu kwamba ulijikita katika vikwazo vya uendeshaji biashara bali pia uliwauliza wafanyabiashara kutaja mambo/maeneo ambayo serikali imefanya vizuri katika suala zima la kuhamasisha uendeshaji wa sekta hiyo.

- Utafiti uliuliza vikwazo vya uwekezaji kwa siku za usoni. Ipo hatari kwa serikali kudhani kwamba wafanyabiashara wataendelea kuwekeza eti kwa sababu ya kuwepo kwa mazingira wezeshi. Ukweli ni kwamba wafanyabiashara hawawezi kuwekeza vitega uchumi bila ya kuwa na uhakika kwa siku zijazo. Iwapo watawekeza ni lazima wawe na imani kwa hali ya vitega uchumi vyao kwa siku zijazo.

- Utafiti umejaribu kuangalia gharama zinazohusika katika uanzishaji wa biashara, hasa taratibu zinazohusika.

- Utafiti huu wa tano, ambao unaonesha kwamba maeneo ya kipaumbele yamebadilika kidogo, kwa mapana unaonesha vipaumbele vilivyowekwa mwaka jana. Maeneo yanahitaji yapewe kipaumbele na serikali siyo tu kuhusu mazingira wezeshi bali pia kukidhi matarajio ya wafanyabiashara.

## 5. Mbinu za utafiti

Utafiti huu ulifanywa na kampuni ya utafiti wa masoko ya Synovate kati ya Juni na Julai 2012.

Utafiti ulifanywa kwa kutumia kitu kinachoitwa ***electronic spreadsheet questionnaire shoulb*** iliyotengenezwa na David Irwin. Kampuni ilichambua matokeo kutoka kwa kila mtu aliyehojiwa. Matokeo hayo yalifanyiwa uchambuzi na David Irwin.

Sampuli ya watu waliohojiwa ni 139 ambao wanajihusisha na biashara mbalimbali za ukubwa na maeneo tofauti.

**Jedwali 3. Watu waliohojiwa**


| Sekta | | Eneo | Ukubwa (Wa-fanyakazi) | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Huduma | 26 | Dar es Salaam | 59 | 0-9 | 69 |
| Kilimo na usindikaji | 21 | Zanzibar | 23 | 10-24 | 52 |
| Viwanda | 23 | Arusha | 19 | 25-49 | 13 |
| Hoteli &Utalii | 26 | Mengine | 38 | 50-99 | 2 |
| Fedha | 23 | BMO | | 100-250 | 1 |
| Mawasiliano | 20 | Mwanachama | 34 | >250 | 2 |
| | | Siyo Mwana-chama | 105 | | |

## 6. Mapitio

Katika swali la kwanza, watu waliohojiwa waliulizwa kueleza mambo muhimu ili kuimarisha biashara zao. Pia walitakiwa kuonesha iwapo jambo hilo lilisababisha uendeshaji wa biashara kuwa mgumu sana, mgumu kiasi, upo uwezekano wa kuboresha au hakuna tatizo kabisa. Inawezekana kabisa kila kigezo kikawa na umuhimu wake. Kwa mfano, mfanyabiashara wa kiwanda atahitaji umeme wa kuaminika au taasisi ya huduma itahitaji mawasiliano ya kuaminika; lakini ili kigezo hicho kisilete matatizo ni lazima kuwepo mawasiliano na umeme wa kuaminika.

Vivyo hivyo, baadhi ya vigezo vinaweza kuwa siyo muhimu. Kwa mfano , rushwa ni lazima ipungue labda tu kama biashara hiyo inategemea rushwa ili iweze kushamiri lakini rushwa inabki ni kikwazo kwa ufanisi wa biashara.
Vigezo vyote vinaonekana ni muhimu. Hakika, ukiondoa rushwa, vigezo vyote vinaonekana ni muhimu kwa asilimia 70 ya watu waliohojiwa. Vigezo sita – umeme, barabara, mawasiliano, usalama, viwango vya kodi na ulipaji kodi – vinaonekana ni muhimu kwa asilimia 95 ya watu waliohojiwa.


**Kielelezo 7: Umuhimu wa vigezo (watu wote waliohojiwa)**




Wafanyabiashara walitakiwa kuonesha vigezo kama vile 'uendeshaji biashara mgumu mno', 'uendeshaji biashara mgumu', 'unaoweza kuboreshwa' au 'siyo tatizo'. Majibu hayo yameainishwa kuanzia 1: siyo tatizo mpaka 4: uendeshaji wa biashara mgumu mno na kuwekwa wastani. Hii inaonesha kwamba masuala muhimu ni umeme, rushwa, viwango vya kodi, ulipaji kodi na upatikanaji fedha.


Kwa mwaka 2011, vigezo vya barabara na maji vilikuwa dhaifu ingawa kwa mwaka 2012 vilionesha hali nzuri. Hali hii haioneshi matatizo kama yalivyobainishwa na Jukwaa la Uchumi Duniani ingawa rushwa, miundombinu na upatikanaji wa fedha yanaendelea kuwa masuala ya kutafutiwa ufumbuzi.


**Kielelezo 8: Mambo yanayosababisha ugumu wa kufanya biashara**



Watu waliohojiwa waliulizwa iwapo ni wanachama wa chama cha wafanyabiashara (BMO). Mwaka 2012, kama ilivyo kwa mwaka 2011, inaelekea kwamba wafanyabiashara waliona vigezo vyote ni vigumu.

**Kielelezo 9: Maoni wanachama wa BMO kuhusu ugumu wa kufanya biashara**





*Katuni imechorwa na Popa Matumula*


Swali moja liliuliza kuhusu vikwazo vya kutolipa kodi. Umuhimu wa vikwazo vya kutolipa kodi ulipungua mwaka 2011 lakini uliongezeka tena katika maeneo matatu: taratibu za mauzo nje, mizani na vikwazo vya barabarani. Si wafanyabiashara wa Tanzania tu wanaolalamika kuhusu masuala ya mizani na vikwazo vya barabarani. Wafanyabiashara wa nchi jirani za Burundi na Rwanda pia wanalalamika kuhusu suala hilo – pamoja na taratibu za kirasimu kwenye mipaka, matatizo ambayo yanasababisha gharama katika uendeshaji biashara. Taratibu za uhamiaji na ulipaji ushuru wa forodha yanaonekana siyo masuala muhimu sana.

**Kielelezo 10: Umuhimu wa vikwazo vya kutolipa kodi (Watu wote waliohojiwa)**




Kwa watu wengi waliohojiwa vikwazo vya kutolipa kodi lilionekana siyo tatizo. Hata hivyo, lazima ieleweke wazi kwamba matatizo yatokanayo na kuwepo kwa vituo vya mizani na vizuizi vya  polisi barabarani yanazidi kuongezeka.


**Kielelezo 11: Vikwazo vya kutolipa kodi vinavyoathiri biashara**




Ingawa vikwazo vya kutolipa kodi vinaweza kuwa ni tatizo kwa wafanyabiashara wadogo, vinaweza kuwa ni tatizo kubwa kwa wafanyabiashara hao katika mazingira yao, hasa iwapo hawajafanya tathmini ya kutosha. Vikwazo hivyo pia vinaweza kuwa na athari kwa wafanyabiashara wanaouza bidhaa zao katika soko la kimataifa.

Umbali hauathiri ukubwa wa tatizo, isipokuwa taratibu za mauzo nje linaonekana ni tatizo kwa upande wa Arusha na vituo vya mizani linaloonekana ni tatizo kwa upande wa wafanyabiashara wa Dar es Salaam.


**Kielelezo 12: Vikwazo vya kutolipa kodi vinavyoathiri biashara**





Watu waliohojiwa waliulizwa mtazamo wao kuhusu jitihada za serikali za kuondoa vikwazo hivi vya mazingira wezeshi. Majibu yao yalikuwa 'serikali inafanya jitihada kubwa kushughulikia kikwazo hicho' (1), 'zipo jitihada' na 'hakuna jitihada' na 'na 'jitihada za serikali zinazidisha tatizo' ( 4). Majibu hayo yakiunganishwa pamoja yanaonesha kwamba idadi kubwa ya watu waliohojiwa wanadhani kwamba kuna maeneo machache ambapo serikali inafanya jitihada kuondoa vizingati vya uendeshaji biashara. Mwaka 2010 eneo la mawasiliano lilionekana kufanikiwa zaidi na kwamba serikali inafanya jitihada katika eneo hilo.

Upatikanaji wa umeme bado ni tatizo ingawa tangu mwaka 2011 hali ni nzuri. Inaonekana kwamba tatizo la rushwa limepungua na kwa mwaka 2012 hali imekuwa mbaya zaidi. Kuna maeneo matatu ambayo utendaji wa serikali unaonekana ni dhaifu sana. Maeneo hayo ni kiwango cha kodi na ulipaji kodi. Eneo jingine ni upatikanaji wa fedha.

**Kielelezo 13: Utendaji wa serikali kushughulikia maeneo muhimu**







*Katuni imechorwa na Idd Marumba*

Tunatarajia kwamba wafanyabiashara ambao ni wanachama wa BMO wataishutumu serikali kutokana na jitihada za serikali kuondoa vikwazo vya uendeshaji wa biashara kwa sababu moja ya sababu kubwa za kujiunga na umoja huo ni kuleta mabadiliko katika sera za umma. Mtazamo huo bado ni hafifu karibu katika maeneo yote. Kwa upande wa upatikanaji wa umeme, wanachama wengi wa BMO wanaishutumu serikali; kwa upande wa tatizo la rushwa, wale wanaoishutumu serikali ni wanachama walioko nje ya BMO.
Idadi ya wanachama kwa kila sekta ni ndogo, kwa hiyo hakuna chochote kinachoweza kuelezwa katika matokeo haya.


**Kielelezo 14: Mtazamo wa wanachama wa BMO kuhusu jitihada za serikali**





Watu waliohojiwa waliulizwa maeneo yanayoweza kuvutia uwekezaji na kwa namna gani (1: kuvutia uwekezaji zaidi; 2: kuvutia au kutovutia; 3: kutovutia uwekezaji). Rushwa ni tatizo kubwa linalozuia uwekezaji, likifuatiwa na

upatikanaji wa umeme. Ingawa yapo mafanikio katika upatikanaji wa umeme, viwango vya kodi, ulipaji kodi na upatikanaji wa fedha bado ni vikwazo vya uendeshaji wa biashara. Maeneo hayo yamepewa ulinganisho wa zaidi ya 2. Haya ndiyo maeneo makuu ambayo yanayokwamisha uwekezaji.

**Kielelezo 15: Mambo yanayogusa maamuzi ya uwekezaji**








*Katuni imechorwa na Idd Marumba*

Kigezo cha 'mazingira wezeshi' kinaunganisha ugumu wa kufanya biashara na jitihada za serikali katika kushughulikia masuala hayo. Kielelezo kifuatacho kinaonesha maoni/mtazamo kwa maeneo yote. Utaona kwamba katika kielelezo hiki yapo mabadiliko kuonesha kwamba kikwazo kikubwa cha uendeshaji biashara kimepewa alama sifuri (0) na kikwazo ambacho serikali imejitahidi kukishughulikia kimepewa alama mia moja (100). Kwa hiyo, kikwazo ambacho kinaonekana siyo tatizo ni mawasiliano, kikifuatiwa na usalama na

wafanyakazi wenye ujuzi. Tatizo kubwa ni upatikanaji wa umeme likifuatiwa na rushwa, viwango vya kodi na ulipaji kodi.

**Kielelezo 16: Kipaumble cha mazingira wezeshi**




Ni vigumu kuunganisha maoni yote katika kielelezo kimoja ingawa tunatambua kwamba katika kielelezo kimoja ni rahisi kuona mara moja iwapo sekta binafsi inabaini kwamba mazingira wezeshi yameimarika au kushuka.

Kwa hiyo, tumetumia kielelezo kimoja kinachoonesha kwamba hali haijabadilika (imeshuka katoka 63.5 mwaka 2011 hadi 62.5 mwaka 2012). Kielelezo hiki kinaonesha kuwa hali, kwa ujumla, haijabadilika.

**Jedwali 4. Mtazamo kuhusu mazingira wezeshi**


| Tanzania | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 |
|---|---|---|---|---|---|
| Burundi | 57 | 65 | 67 | 63 | 63 |
| Kenya | 52 | 56 | | | |
| Rwanda | | 76 | | | |
| Uganda | 63 | 59 | | | |

Kwa wasomaji wanaopenda kupata maelezo ya kina wanaweza kupata maelezo hayo toka BEST-AC kwa kila eneo. BEST-AC wanaweza kutoa takwimu kuhusu ukubwa wa kila taasisi ya biashara

## 7. Tathmini mahali ilipo biashara

Kwa ujumla, wafanyabiashara wa Zanzibar wanaona ugumu wa kuendesha biashara wakati wale wa Dar es Salaam wanaona ni rahisi kuendesha biashara zao. Upatikanaji wa umeme na rushwa ndiyo matatizo makubwa katika visiwa hivyo. Upatikanaji wa fedha na usajili wa ardhi ndiyo matatizo makubwa kwa upande wa Arusha. Wafanyabiashara wa Arusha pia wanalalamika kuhusu barabara mbovu, leseni na sera za uchumi.

**Kielelezo 17: Vikwazo kwa kila eneo la kjiografia**





## 8. Gharama za urasimu

Duniani kote wafanyabiashara wanalalamika kuhusu gharama za urasimu - hasa gharama za kushughulikia leseni na taratibu nyingine za kimaandishi.

Watu waliohojiwa waliulizwa kuhusu gharama za taratibu mbalimbali katika makundi matatu: gharama za kupata leseni, ikiwemo gharama ya kupata leseni zenyewe, muda wa kukamilisha taratibu hizo kimaandishi na namna ya kushughulika na watekelezaji wenyewe. Watu waliohojiwa waliulizwa ni katika kundi gani hasa kulikuwepo gharama kubwa zaidi.


Mwaka 2009, asilimia 20 ya watu waliohojiwa walisema kuna gharama kidogo au hakuna gharama kabisa katika kila eneo. Kufikia mwaka 2012, hakuna mtu hata mmoja yeyote aliyethubutu kusema kwamba hakuna gharama kabisa.

**Kielelezo 18: Gharama urasimu na taratibu**




Kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, watu wengi waliohojiwa walisema kwamba kila eneo lilihitaji matumizi ya asilimia tatu. Hiki kinaonekana ni kiwango kidogo ingawa ukiunganisha maeneo yote kiasi hicho kinakuwa kikubwa zaidi. Kielelezo kifuatacho kinaonnesha wastani wa matumizi kwa sekta hizo tatu.
Kielelezo

**19: Gharama za urasimu na taratibu**




Wafanyabiashara wanasema gharama ni kubwa mno Arusha na ndogo sana Zanzibar.

**Kielelezo 20: Ulinganisho wa kijiografia kuhusu gharama za uendeshaji biashara**




Jitihada za kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara zitasaidia kuokoa rasilimali ambazo wafanyabiashara watazitumia kuwekeza katika biashara zao, hasa kwa lengo la kutoa ajira na kuchochea shughuli za kiuchumi. Kwa njia hiyo, serikali itajipatia mapato ya kutosha na kila mtu atakuwa ni mshindi.

## 8. Kodi

Tathmini iliyofanyika mwaka 2012 iliangalia mfumo wa kodi nchini Tanzania, hasa kwa kuangalia sera za kodi za serikali na kiwango cha kodi kinachopotea kutokana na ukwepaji, mitaji na misamaha ya kodi (Curtis 2012). Kutokana na kutoridhishwa na hali halisi ya ulipaji kodi ndiyo maana tathmini hii ilionesha kwamba haishangazi kuona taasisi mbalimbali zinaripoti asilimia 69 tu ya mauzo yao na kwamba asilimia 40 ya taasisi zisizo rasmi hazilipi kodi kabisa ingawa baadhi ya taasisi hizo ni ndogo mno kulipa chochote. Kwa ujumla tathmini inaonesha kwamba serikali hukusanya kiasi cha dola za Marekani bilioni 1.3 kwa mwaka, makusanyo ambayo ni kidogo mno. Kiasi hicho ni sawa

na 1/6 ya bajeti ya serikali. Tathmini inatoa mapendekezo kadhaa kwa serikali katika kurekebisha sera zake za kodi katika jitihada zake za kukusanya mapato inayostahili.

Lazima kutakuwepo na wafanyabiashara na watu binafsi ambao watajitahidi kubuni kila mbinu ili waweze kukwepa ulipaji kodi ingawa wafanyabiashara wengi wanatambua umuhimu wa kulipa kodi ili serikali iweze kuwa na mapato kwa matumizi yake. Hata hivyo, wafanyabiashara hao wanataka kuona matokeo mazuri kutokana na matumizi ya serikali.

Kwa hiyo, ripoti inasisitiza umuhimu wa mapendekezo ya kurahisisha mfumo wa kodi (hii pia itapunguza vitendo vya rushwa) na kuongeza uwazi katika ukusanyaji kodi na katika matumizi ya serikali. Mfumo wa kodi ni budi ujengwe katika misingi ya kutopendelea baadhi ya wafanyabiashara iwapo kodi itakusanywa kwa ufanisi zaidi ili kupunguza ulipaji wake kwa wafanyabiashara wote.

Ingawa upatikanaji wa umeme bado ni changomoto kubwa kwa upande wa serikali, tayari zipo jitihada za makusudi zinazofanyika kutatua tatizo hilo. Serikali ni lazima ifanye kila jitihada kupambana na tatizo la rushwa. Njia nzuri ya kupambana na tatizo hilo, kama inavyotambulika, ni kuziba mianya ya rushwa. Changamoto mbili zilizobainishwa na utafiti wa hivi karibuni wa maoni ya wafanyabiashara ni viwango vya kodi na ulipaji kodi wenyewe. Changamoto hizi mbili ni rahisi kuzishughulikia na kuleta mabadiliko siyo tu kwa mtazamo wa serikali kuhusu sekta ya biashara bali pia katika kuhakikisha serikali inakusanya mapato yake.

**Rejea**

Curtis, M (2012), The one billion dollar question: how can Tanzania stop losing so much tax revenue, Tanzania Episcopal Conference, National Muslim Council of Tanzania and Christian Council of Tanzania

Schwab,K, (2011), *The Global Competitiveness Report 2011-2012, W*orld Economic Forum

Schwab,K, (2012), *The Global Competitiveness Report 2012-2013, World Economic Forum*

*Transparency International, Corruption Perception Index, available at http://cpi.transparency.org/cpi2012/results/#myAnchor2*


*World Bank (2008), Doing Business 2009*

*World Bank (2009) Doing Business 2010: reforming through difficult times*

*World Bank (2010), Doing Business 2011: making a difference for entrepreneurs*

*World Bank (2011), Doing Business 2012: doing business in a more transparent world*

World Bank (2012) Doing Business 2013: smarter regulations for small and medium sized enterprises




**BEST-AC**
**P.O.BOX 6983 Dar es Salaam - Tanzania**
**Simu: +255 022 2601168**
**Barua Pepe: info@best-ac.org | Tovuti: www.best-ac.org**

BEST-AC Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy